**East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature**

OPEN ACCESS

*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya

Volume-7 | Issue-12 | Dec- 2024 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2024.v07i12.007

**Original Research Article**

# Ubainishaji wa Dhima Zilivyojitokeza Kupitia Vipengele vya Ushikamani wa Darajia ya Kisarufi Kupitia Tamthiliya ya *Natala* na *Morani*

Allen Estomih Makyara[1*], Neema George Mturo[1]

[1]Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Makumira, Tanzania

**Article History**
**Received:** 11.08.2024
**Accepted:** 25.11.2024
**Published**: 30.12.2024

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala hii imebainisha dhima zilivyojitokeza kupitia vipengele vya ushikamani wa darajia ya kisarufi katika tamthiliya ya *natala* (Kithaka Wa Mberia, 1997) na *morani* (Emanuel Mbogo, 1993). Makala hii yalitumia mkabala wa kimaelezo na usampulishaji lengwa. Usanifu unahusu tafiti zinazolenga kuchunguza jambo fulani kwa kina. Data zilikusanywa kutoka maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kusimbisha maudhui. Mjadala wa matokeo ya utafiti uliongozwa na nadharia ya Ushikamani iliyoasisiwa na Halliday na Hassan (1976). Hivyo matokeo ya makala yalionyesha kuwa matini na kazi mbalimbali za kifasihi huweza kuwa na ushikamani wa mawazo endapo vipengele vya darajia ya ushikamani wa kisarufi vitazingatiwa na kufuatwa, ili ziweze kuwa na ushikamani wenye kuleta mtiririko mzuri wa mawazo. Hata hivyo katika upande wa dhima za darajia ya ushikamani wa kisarufi matokeo yalionesha kuwa dhima hizi zinasaidia kuleta mtiririko wa matini ambao ni wa kueleweka kwa wasomaji au wasilikilizaji (Halliday na Hassan, 1976). Kwa hiyo matini haiwezi kuwa matini bila ya sentensi zake kushikamana sawasawa. Hivyo darajia ya ushikamani ni nguzo katika kazi za fasihi kwani huleta mtiririko mzuri wa mawazo kwa kuwa kazi nyingi zikikosa ushikamani zinakosa maana iliyokusudiwa.

**Keywords:** Ushikamani, Ushikamani wa kisarufi.

**Copyright © 2024 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Halliday na Hassan (1976:4) wanasema ushikamani ni dhana ya kisemantiki, na hurejelea uhusiano wa maana uliopo katika matini. Ili matini yoyote iwe na maana na kueleweka na wasomaji lazima iwe na ushikamani. Hivyo kwa ujumla tunaweza kusema kuwa Ushikamani ni hali ya vipashio fulani katika sentensi au matini kukaa pamoja kwa uimara. Kwa hiyo tunaona swala la ushikamani ni la muhimu katika kazi yoyote ya fasihi kwani ndiyo nguzo kuu katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Katika fasili hii, tunaona kwamba katika lugha kuna vijenzi ambavyo huonesha uhusiano wa neno kwa neno ili kuunda sentensi, na pia sentensi kwa sentensi ili kuunda aya, na kupelekea kupatikana kwa matini nzima yenye kuleta maana. Kwa mantiki hii, tunaona kuwa, matini haiwezi kuwa matini bila ya sentensi zake kushikamana sawasawa, ili kujenga maana yenye kufahamika na kujulikana hiyo matini ni ya nini au inazungumzia kitu gani.

Hivyo makala hii yataenda kuchunguza ubainishaji wa dhima zilivyojitokeza kupitia vipengele vya ushikamani wa darajia ya kisarufi kupitia tamthiliya ya *natala* na *morani*. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), anafafanua Ushikamani wa kisarufi ni hali ya kushikana kwa sentensi katika matini kupitia vijenzi vya urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji wa elementi mbalimbali katika matini ili kuleta muwala na maana; akiendelea kufafanua vipengele hivyo vitokanavyo na ushikamani anaeleza Kirejelewa ni elementi katika sentensi au matini ambayo imerejelewa na kiwakilishi; hata hivyo Kibadala ni neno linalosimama badala ya kitenzi au nomino au dhana katika matini; vilevile Kidondoshwa ni nomino au kitenzi au kirai au kishazi au sentensi au msururu wa sentensi uliodondoshwa katika matini. Kiunganishaji ni aina ya uhusiano wa kimaana katika matini, ambao huunganisha mpangilio wa matukio yanayoelezewa na vipashio vya kiisimu.

Ushikamani wa darajia ya kisarufi ni msingi wa kimuundo unaoelezea jinsi dhima mbalimbali zinavowekwa na kutambulika ndani ya sentensi na matini kwa ujumla. Dhima kwa upande wake zinaweza kueleweka vizuri zaidi kupitia muundo na ushikamani wa kisarufi wa lugha husika. Kwa mujibu wa Mkude (2005), anafafanua kuna dhima za ushikamani wa darajia

***Corresponding Author:** Allen Estomih Makyara
Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Makumira, Tanzania

ya kisarufi ni muhimu katika kuhakikisha uelewa, muundo na usahihi wa lugha ya Kiswahili. Hivyo katika makala haya tutachunguza dhima za ushikamani wa darajia ya kisarufi na namna zinavyoweza kutumika katika tamthiliya ya *Natala* na *Morani*.

## 2.0 METHODOLOJIA

Sehemu hii imehusisha mkabala wa utafiti, usanifu wa utafiti, usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na itikeli.

### 2.1 Mkabala na Usanifu wa Utafiti

Katika makala haya tumetumia mkabala wa kimaelezo katika kuzichambua data zilizokusanywa kutoka maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Katika makala haya mtafiti alitumia usanifu wa kifani kwa lengo la kubainisha vipengele vya darajia ya Ushikamani wa kisarufi na namna vinavyoibua dhima katika Tamthiliya ya *Natala* na *Morani*.

### 2.2 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti uliofanikisha makala haya ulitumia sampuli ya tamthiliya mbili tamthiliya ya *Natala* (1997) iliyoandikwa na mwandishi Kithaka wa Mberia na tamthiliya ya *Morani* (1993) iliyoandikwa na mwandishi Emanuel Mbogo.

### 2.3 Mbinu za Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data

Data za makala haya zilikusanywa kutoka maktabani. Mtafiti alitumia mbinu ya uchanganuzi matini kwa kusoma tamthiliya ya *Natala* na *Morani*. Pia Data zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu za kusimbisha maudhui. Katika makala haya mtafiti alizingatia hatua za uchanganuzi wa data. Kwanza kuzizoea data kwa kuzisoma. Data zilikusanywa kutoka kitabu cha tamthiliya ya *Natala* na *Morani*. Pili mtafiti alitengeneza misimbo mbalimbali kwa kuzingatia malengo mahususi, matukio, mipango, maana, uhusiano na hali. Tatu mtafiti aliunganisha misimbo iliyolandana ili kuunda sura fulani ya kimaudhui.

## 3.0 MATOKEO YA UTAFITI NA MJADALA WA MATOKEO

Sehemu hii inawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa ili kukidhi lengo la utafiti katika makala haya. Lengo kuu ni ubainishaji wa dhima zilivyojitokeza kupitia vipengele vya ushikamani wa darajia ya kisarufi kupitia tamthiliya ya *Natala* na *Morani*. Hivyo matokeo ya makala haya yalionyesha kuwa matini na kazi mbalimbali za kifasihi huweza kuwa na ushikamani wa mawazo endapo vipengele vya darajia ya ushikamani wa kisarufi vitazingatiwa na kufuatwa, ili ziweze kuwa na ushikamani wenye kuleta mtiririko mzuri wa mawazo kwa kuwa kazi nyingi zikikosa ushikamani zinakosa maana iliyokusudiwa.

### 3.1 Ubainishaji wa Dhima Zilivyojitokeza Kupitia Vipengele vya Ushikamani wa Darajia ya Kisarufi Kupitia Tamthiliya ya *Natala* na *Morani*

Katika sehemu hii tumewasilisha data zinazohusu vipengele vya darajia ya Ushikamani wa kisarufi katika Tamthiliya ya *Natala* na *Morani*. Data zimewasilishwa na kuchambuliwa kulingana na lengo husika. Hivyo Vipengele vya darajia ya ushikamani wa kisarufi vilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani* ni kama ifuatavyo:

#### 3.1.1 Urejeleaji

Urejeleaji ni mojawapo wa kijenzi cha ushikamani wa kisarufi kilichotumika katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani*. Kijenzi hiki hutumika ili kuepusha urudiaji wa maneno katika matini. Nomimo (kiima) haiwezi kurudiwa katika matini mara kwa mara, bali hutumika kiwakilishi chake ili kuiwakilisha nomino hiyo pindi inapojitokeza kwa mara nyingine. Katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani* mwandishi ametumia urejeleaji/urejelezi katika darajia ya ushikamani wa kisarufi ambapo mwandishi anasema:

**Kwa upande wa kitabu cha Natala:**
**Mf. 1**
**Gane:** *Njema. Watoto wako wapi? Nina ujumbe* ***wao.***
**Natala:** *Wanacheza uani.*
**Gane:** *Sikuwaona.*
**Chanzo**; (Mberia, 1997:1)

**Mf. 2**
**Chifu:** *Nina ujumbe wenu* ***wewe na yeye****.*
**Natala:** *Ngoja nimwangalie kwake.*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:8)

**Kwa upande wa kitabu cha Morani:**
**Mf1**:
**Aisha:** *Nikopeshe basi!*
**Okasha:** *Mtu mazishi kama* ***wewe*** *akukopeshe nani! (Anaonyeshea kwa Malongo)*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:32)

**Mf2***:*
**Mapoto:** *Unauliza kama humjui Dongo?*
**Malongo:** *Ni hatari.*
**Jalia:** *Na* ***yeye*** *pia anafahamu kuwa ni hatari. Lakini aliniambia hawezi kujificha na kusaliti umma wakati huu wa damu.*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:41)

Matokeo yalionyesha kuwa Urejeleaji ni kijenzi kimojawapo cha ushikamani kama ilivyoshadidiwa na Salkie, (1995); Halliday, (1985); Halliday na Hassan, (1976) ambapo wanaeleza kuwa kijenzi hiki hutumika ili kuondoa urudufishaji wa maneno katika matini. Nomino (kiima au yambwa) haiwezi kurudiwa katika matini kila mara bali kiwakilishi nomino, mfano mimi, yeye, hutumika kuwakilisha nomino hiyo pindi inapojitokeza mara ya pili (Halliday, 1985); Pia Barongo (1996)

akiendelea kufafanua anasema Urejeleaji ni ile hali ya kuwa msomaji wa matini inambidi arejelee elementi nyingine katika matini ili kupata mshikamano wa sentensi au matini na kuleta maana inayoeleweka au iliyokusudiwa. Hivyo kwa kuongozwa na nadharia ya Ushikamani katika muhimili wa kwanza tunaweza kuona jinsi Ishara na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wa maana na kila mmoja ndani ya muktadha wa lugha. Hivyo kijenzi hiki kiliweza kutumika ili kuepusha urudiaji wa maneno katika matini, ambapo mara nyingi huweza kujitokeza katika matini. Matokeo yalidhihirisha kuwa Kijenzi hiki kilitumika ili kuepusha urudiaji wa maneno katika matini ambapo Nomimo (kiima) haiwezi kurudiwa katika matini mara kwa mara, bali hutumika kiwakilishi chake ili kuiwakilisha nomino hiyo pindi inapojitokeza kwa mara nyingine.

**3.1.2 Ubadilishaji/Ubadala**

Ubadala ni neno linalosimama badala ya kitenzi au nomino au dhana katika matini. Hii ni aina ya ushikamani inayohusisha vipengele mbalimbali vya kiisimu kwa maana kwamba kile kinachofuata chenzie ni kibadala ya kile kilichotangulia. Hivyo Ubadilishaji/Ubadala ni mchakato katika matini ambapo hutokea ubadilishaji wa kipashio kimoja na kuingiza kipashio kingine. Hivyo data ilionyesha kipashio kinachosimamia kingine, tunakiita kibadala. Katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani* mwandishi ametumia ubadala/ubadilishaji katika darajia ya ushikamani wa kisarufi ambapo mwandishi anasema:

**Kwa upande wa kitabu cha Natala:**
**Mf1:**
**Tila:** *Natala, hutaniongezea chumvi.*
**Natala**: *Ningekuongezea ila sina uwezo wa kufanya **hivyo.***
**Chanzo;** (Mberia, 1997:4)

**Mf2:**
**Kasisi:** *[Akiwatangazia watu wote] Tuombeni! Mungu baba, kwa nyoyo ambazo zimefunuka, kwa mikono ambayo imeenyooka, na kwa imani imara kama mwamba, tunakuomba umkubali **huyu** mwanao katika utukufu wako.*
**Watu wote:** *Amina!*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:27)

**Kwa upande wa kitabu cha Morani:**
**Mf1***:*
**Mlemeta:** *Nani?*
**Yusufu:** *(Kwa kukazia) Jalia!*
**Mlemeta:** *Hana lolote **huyu**.*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:15)

**Mf2**:
**Jalia:** *Basi tuache. Labda Dongo mwenyewe hawezi kukubali, kama wote mwaona **hivyo**, basi tuache.*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:42)

Matokeo yameonyesha dhana ya ubadala ni mchakato katika matini ambapo hutokea ubadilishaji wa kipashio kimoja na kuingiza kingine, ambapo ikijadiliwa na Halliday na Hassan 1976 wanasema kuwa Ubadilishaji hutokea katika matini kwa kuweka elementi moja badala ya nyingine ambayo ilitumika katika sentensi iliyotangulia. Hivyo kwa kuongozwa na nadharia ya ushikamani ni dhahiri kuwa ishara na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wa maana na kila mmoja ndani ya muktadha wa lugha. Kwa mfano, sentensi nzima inapaswa kuwa na uhusiano wenye maana na maneno yake yote, na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wenye maana na vitu vinavyowakilisha. Hivyo matokeo yalionyesha kuwa ubadilishaji au ubadala huondoa urudufishaji katika kiswahili, na kuleta mshikamano unaofaa. Matokeo yalionyesha maneno kama; "*hivyo", "ileile", "huyu", "hicho", "huu"* yalitumika katika matini kwa lengo la kuwakilisha maneno mengine. Hivyo ubadilishaji ni muhimu katika matini za Kiswahili kwa kuondoa urudufishaji na kudhibiti mshikamano wa matini.

**3.1.3 Udondoshaji**

Udondoshaji ni kuacha au kuondoa elementi fulani katika matini na kuonesha kuwa urudiaji wake si muhimu katika sentensi inayofuata. Aghlabu kinachoweza kudondoshwa katika matini ni nomino, kitenzi au kishazi. Data zilionyesha mwandishi hawezi kudondosha atakavyo kwani anapofanya hivyo atapoteza maana na mshikamano wa matini. Katika tamthiliya ya *Natala* na *morani* mwandishi ameonyesha udondoshaji katika darajia ya ushikamani wa kisarufi ambapo mwandishi anasema:

**Natala**:
Mf1; Natala: *Namaanisha watu wanaosubiri maiti ya marehemu (**Mume wangu**)* Uk 21

Mf2; Gane: *Ndio. (**Watoto**) wanapenda sana kucheza na kuimba.*Uk. 23

**Morani**:
Mf1; Mlemeta: *Kesho saa nne usiku twende kwake. (**Nungunungu**)* Uk. 15

Mf2; Nungu: *(Hasira zinampanda) Sikiliza Aisha! Usiniletee utoto mimi. (**Aisha**) kitu gani kimekufukuzisha shule. (Kimya) Husemi?* Uk 26

Matokeo yalionyesha udondoshaji ni kuacha au kuondoa elementi fulani katika matini na kuonesha kuwa urudiaji wake si muhimu katika sentensi inayofuata. Maelezo hayo yanamaanisha kwamba, hakuna haja ya kutaja elementi kwa mara ya pili au zaidi, kwa sababu elementi hiyo hufikiriwa katika muktadha uliopo hivyo udondoshaji hutokea kwa kuondoa urudufishaji. Udondoshaji huu ulijitokeza kwa kudondoshwa neno zima katika sentensi. Akiendelea kuielezea Halliday na Hassan, (1976) wanasema kuwa Udondoshaji ni miongoni mwa aina ya ushikamani ambayo hujitokeza

pale ambapo baadhi ya elementi katika sentensi huondolewa au huachwa kutumiwa katika sentensi kutokana na sababu mbalimbali bila ya kuathiri maana. Udondoshaji ni utaratibu wa kutoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi (Massamba 2004). Udondoshaji ni seti ya rasilimali ambayo hufanya urudiaji wa kishazi au elementi fulani kuepukwa, na kudokezwa kwa wasomaji kuwa warejelee kishazi au elementi iliyotangulia ili kukamilisha maana (Thompson 2004). Toolan (1998), alieleza kuwa udondoshaji ni kijenzi cha pili kwa ukubwa katika vijenzi vya ushikamano. Hivyo kwa kuongozwa na nadharia ya ushikamani tumeweza kuona kuwa udondoshaji ishara na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wa maana na kila mmoja ndani ya muktadha wa lugha. Kwa mfano, sentensi nzima inapaswa kuwa na uhusiano wenye maana na maneno yake yote, na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wenye maana na vitu vinavyowakilisha. Hata hivyo Dhana ya udondoshaji imejitokeza pia kama mojawapo ya mkakati wa kukidhi vigezo vya tafsiri ya mazungumzo. Kwa mujibu wa Koolstra na wenzake (2002), Cronin (2009), Ching Ting (2010), Chang (2012) na Mogadam na Shabanipoor (2013) udondoshaji ni mkakati mmojawapo wa kufanikisha tafsiri ya mazungumzo kutokana na kwamba inaondoa mambo yote ambayo si ya muhimu katika sentensi ili kukidhi sheria na kanuni za idadi ya mistari na herufi katika kiwambo. Hivyo matokeo yalionyesha kuwa udondoshaji ulisababishwa na urudufishaji wa neno. Hujitokeza pale ambapo neno au maneno katika matini kulazimika kudondoshwa pale linapojitokeza zaidi ya mara moja ili kupunguza uradidi usio na msingi. Aidha, udondoshaji wa urudufishaji wa maneno yenye uhusiano humaanisha kuwa neno au maneno huweza kudondoshwa iwapo kuna mwingiliano wa maana baina ya maneno hayo. Hivyo, hata maneno hayo yakidondoshwa maana zake zitabebwa na maneno au vipashio vinavyosalia.

### 3.1.4 Uunganishaji

Data zilionyesha kuwa uunganishaji ni kule kuunganisha vipashio viwili au zaidi na wakati mwingine kipashio kimoja huwa tegemezi. Hii ni kusema kwamba, maana mbili zinapoungana huunda mantiki katika matini. Katika lugha ya kiswahili kuna viunganishi vya aina mbili navyo ni viunganishi ambatanishi na viunganishi tegemezi.

#### 3.1.4.1 Viunganishi ambatanishi

Viunganishi ambatanishi ni maneno au vifungu vya maneno vinavyounganisha sentensi, vifungu vya maneno au maneno ndani ya sentensi moja. Hivi viunganishi vinaweza kugawanywa navyo katika makundi mawili nayo ni viunganishi ambatanishi dhahiri na viunganishi ambatanishi si dhahiri; ila katika data zetu tutajikita katika viunganishi ambatanishi dhahiri ambavyo viko katika makundi matano kama ifuatavyo:

##### 3.1.4.1.1 Viunganishi ambatanishi viongezi

Viunganishi ambatanishi viongezi ni aina ya uunganishaji ambao huongeza jambo, tukio fulani au habari kwa kutumia viunganishi na kuleta ushikamano katika matini. Data zilionyesha kuwa viunganishi vinavyotumika hapa ni kama "*na", "au", "ama", "zaidi ya", "wala", "tena", "pia", "p*

**Kwa upande wa kitabu cha Natala:**
**Natala:** *Nakubaliana nawe. Na ukweli unaotaja unanihusu mimi moja kwa moja. Vitendo vyangu,* ***zaidi ya*** *maneno yangu, ni Ushahidi wa ukarimu wangu.*
**Tila:** *Natala, hutaniongeza chumvi.*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:4)

**Mf2***:*
**Gane:** *Ndio. Wanapenda sana kucheza* ***na*** *kuimba. Hivi punde walikuwa wanacheza humu ndani. Baada ya Mzee Balu kuingia nikawaambia waende wakacheze nje.*
**Chanzo:** (Mberia, 1997:23)

**Mf1**:
**Malongo:** *(Kwa Okasha) Tuletee bia moja* ***na*** *soda moja*
**Okasha.** *(Kimya Okasha anamimina bia kisha soda)*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:34)

**Mf2**:
**Malongo:** *Wanacheka nini? Wanacheka nini? Nimeeleza* ***juu ya*** *ushenzi wa yule jaji mahakamani. Kitu gani cha kuchekesha?*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:36)

**Viunganishi vichaguzi**

Viunganashi vichaguzi hutumika katika tungo ili kuchagua jambo moja kati ya mambo mawili kutokana na jinsi yaliyoambatanishwa. Data zinaonyesha kuwa Viunganishi vichaguzi huwakilishwa kwa kutumia viunganishi kama; ""*au"*, "*ama"*, na "*labda*" Mfano kutoka katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani*, mwandishi ameonyesha viunganishi vichaguzi katika darajia ya ushikamani wa kisarufi Mwandishi anasema:

**Kwa upande wa kitabu cha Natala:**
**Mf1, Tila:** *Unawezaje kutia sukari* ***au*** *mafuta ya taa katika chakula? Uk3*
**Mf2, Natala:** *Tila, ulikuwa umekuja kuomba chumvi* ***au*** *ulikuwa na mengine? Uk. 4*

**Morani:**
**Mf1**
**Dongo:** *Siyo kitu. Nikusomee orodha ya madhambi yake* ***au*** *unayajua yote? Uk. 12*

**Mf2**
**Jalia:** *Wala msiwafanye wananchi wajinga* ***au*** *hawaoni. Uk 14*

**Viunganishi ambatanishi Vichaguzi**

Viunganishi ambatanishi Vichaguzi ni aina ya viunganishi ambatanishi ambavyo huashiria hali ya utenguzi au ukinzani wa maana. Hii ni aina ya uunganishaji ambao hutokea wakati viunganishi vinatumika kuunganisha mawazo, dhana au maana katika matini, Mfano kutoka katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani* mwandishi ameonyesha viunganishaji ambatanishi vichaguzi katika darajia ya ushikamani wa kisarufi ambapo mwandishi anasema:

**Kwa upande wa kitabu cha Natala:**
**Mf1**:
**Gane:** *Amini nisemayo, Natala.*
**Natala:** *Najaribu, **lakini** nina wasiwasi na hofu. [Anajifunika uso kwa viganja] Ewe kifo, kwanini? Kwanini mapema namna hii?*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:23)

**Mf2**:
**Gane:** *Nilimwona akitoka huku jana nikafikiria **labda** mmeazima mvo uliokuwepo baina yenu.*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:40)

**Mf1**:
**Dongo:** *Kwani vipi? Kwani meno yalikuwa yamekamatana, ndimi zimekatwa na utomvu umekauka. **Hata hivyo** manusura ya macho yao yenye mwana hafifu yaliwatia moyo kuendelea kupapasa, kuitafuta njia.*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:7)

**Mf2**:
**Aisha:** *Kwa vipi?*
**Okasha:** *Maana unaonekana upo **lakini** haupo.*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:32)

**Viunganishi Ambatanishi Kanushi**

Viunganishi ambatanishi kanushi katika tamthiliya hizi vimetumika kuambatanisha kipashio kwa kuonyesha hali ya ukanushi yaani hakuna kinachochaguliwa baina ya vitu viwili katika tungo. Mfano kutoka katika tamthiliya ya *Natala* na tamthiliya ya *Morani* mwandishi ameonyesha viunganishaji ambatanishi kanushi katika darajia ya ushikamani wa kisarufi Mwandishi anasema:

**Kwa upande wa kitabu cha Natala:**
**Mf1**: ***Natala**: Mwanamke si mpumbavu na **wala** si gogo la mgomba. Uk 19*

**Morani:**
**Mf1:**
*Malongo: Nakuambia Mapoto, paka hawezi kupigana na chui.*
*Mapoto: **Siyo** kila siku…wakati mwingine anaweza. Uk 35*

**Viunganishi Ambatanishi vya Wakati**

Uunganishaji huu huonesha jinsi wakati unavyounganisha sentensi mbili au zaidi na aya katika matini. Aina hii ya uunganishaji huonesha wakati ambao jambo fulani limetokea, na baadae jambo jingine kutokea au likafuatia. Kwa hivyo kinachounganishwa ni yale matukio au mambo yaliyojitokeza kwa kutumia kiunganishi cha wakati. Katika tamthiliya ya *Natala*, mwandishi ameonesha viunganishi vya wakati katika darajia ya ushikamani wa kisarufi kwa kusema:

**Mf1***:*
**Natala:** *[Kutoka sakafuni] kabla ya machozi kunikauka, mengine yananitiririka! **Kabla ya** majeraha kupona, moyo umepata mengine!*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:10)

**Mf2:**
**Natala:** *Ndio, mume wangu, ningekushika mkono na kukuinua, na kufukuzia mbali ujane wang una uyatima wa Watoto wangu. Laiti ningekuwa nayatamka maneno mengine, **badala ya** haya mawili: Ujane na Uyatima.*
**Chanzo;** (Mberia, 1997:32)

**Kwa upande wa kitabu cha Morani:**
**Mf1: Dongo:** *Naitaka hiyo orodha **baada ya** dakika kumi (Anaweka simu chini. KIMYA kidogo) Kila mahali wameweka watu. Laki… (Sauti ya bundi) Ndege?*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:8)

**Mf2: Mzee**: *Amkeni amkeni! (Mapoto anaamka **kabla ya** Malongo) Amkeni Amka Malongo!*
**Chanzo;** (Mbogo, 1993:3)

**Viunganishi Tegemezi.**

Data zinaonyesha kuwa viunganishi tegemezi ni aina ya viunganishi vinavyotumiwa kuunganisha sentensi mbili au zaidi ambapo sentensi moja inategemea nyingine ili kuwa na maana kamili. Viunganishi hivi vinaonyesha uhusiano wa utegemezi kati ya sentensi hizo. Kwa mfano, moja inaweza kuwa sababu ya nyingine, au moja inaweza kutokea baada ya nyingine. Katika tamthiliya ya *Natala* mwandishi ameonesha viunganishi tegemezi katika darajia ya ushikamani wa kisarufi anaposema:

**Morani:**
**Mf1: Gane:** *Siondoki **kwasababu** ya kufukuzwa. Naondoka **kwasababu** nina haraka. Kwaherini. [Anaondoka] Uk.3*

Matokeo yalionyesha uunganishaji ni aina mojawapo ya vijenzi vya ushikamano vilivyotumiwa na waandishi wa riwaya hizi teule, ili kushikamanisha sentensi na msomaji aweze kuelewa kilichokusudiwa. Halliday na Hassan (1976) wamesema kuwa uunganishaji ndio aina pekee ya ushikamano ambayo daima huunganisha maana ya vishazi na sentensi kama kazi kwa ujumla.

Hii ni kusema kwamba, maana mbili zinapoungana huunda mantiki katika matini. Naye O'grady na wenzake (1996) wakizungumzia kuhusu uunganishaji wamesema kuwa, viunganishi hutumika

kuunganisha elementi au kategoria za kisintaksia mbili au zaidi. Wakifafanua zaidi wameeleza kuwa, viunganishi vya nomino au vitenzi vinaweza kudondoshwa isipokuwa kile kinachotokea kabla ya nomino au kitenzi cha mwisho. Maelezo haya yanamaanisha kuwa, ikiwa kuna viunganishi vinavyounganisha nomino au vitenzi kadhaa vinavyofuatana, viunganishi vinavyotokea awali vinaweza kudondoshwa isipokuwa kile kiunganishi cha mwisho.

Hata ikiwa viunganishi hivi vikidondoshwa, ushikamano bado utakuwepo katika matini na maana itapatikana. Uunganishaji ni ile hali ya kuunganisha dhana au maana au elementi mbalimbali katika sentensi au matini kwa kutumia viunganishi (Makoti 2013). Hivyo, matokeo yanathibitika wazi katika uunganishaji kipashio kimoja huwa tegemezi ya kingine katika matini kama data zilivyokuwa zikionyesha ambapo vipashio viwili au zaidi huweza kuunganishwa kwa kiunganishi.

Kwa hiyo uunganishaji ni njia moja ya kushikamanisha mawazo, dhana, vitendo au elementi mbalimbali katika sentensi au matini kwa kutumia viunganishi vya aina mbalimbali ili kuleta maana inayofahamika kwa msomaji. Kwa kuongozwa na nadharia ya ushikamani tunaweza kuona kuwa uunganishaji ni hali ya vipashio fulani (katika sentensi au matini) kukaa pamoja kwa uimara kama ilivyoweza kushadadiwa na Finch, (2000). Anasema kuwa ili matini, yoyote iweze kuwa na maana na kueleweka na wasomaji, lazima iwe na ushikamani ambao tuliweza kuupata katika kijenzi hiki cha uunganishaji.

### 3.2 Dhima za Vipengele vya Darajia ya Ushikamani wa Kisarufi Katika Tamthiliya ya *Natala* na *Morani.*

Dhima za darajia ya ushikamani wa kisarufi ni mbinu au njia zinazotumika katika lugha ili kuhakikisha kwamba maandishi au matamshi yanaunganika vizuri na kuwa na mtiririko mzuri. Zifuatazo ni baadhi ya dhima kuu za darajia ya ushikamani wa kisarufi:

#### 3.2.1 Kuondoa Hali ya Uradidi

Data zilionyesha kuwa hii ni mbinu ya kutumia maneno au vifungu kuashiria maneno au vifungu vingine vilivyotangulia au kufuata katika maandishi. Urejeleo husaidia kuepuka kurudia rudia maneno yale yale mara kwa mara; hivyo kuweza kuondoa hali ya uradidi katika matini. Aidha uradidi ukizidi humfanya msomaji wa tamthiliya aone kazi haina mvuto na haikuzingatia kanuni za utunzi. Hata hivyo kijenzi hiki hutumika ili kuepusha urudiaji wa maneno katika matini.

Matokeo yalionyesha kuwa mbinu ya kutumia maneno au vifungu vya maneno au vifungu vingine vilivyotangulia au kufuata katika maandishi vimeweza kutumika kupitia viwakilishi kama vile "*yeye,*" "*wao,*" "*hicho*," na "*hivyo*,". Urejeleo husaidia kuepuka kurudia rudia maneno yale yale mara kwa mara. Matokeo yanaonyesha pia Urejeleaji huwa na vitambulishi vyake. Kazi ya vionyeshi vya urejeleaji huwa viwakilishi na pia huwa vionyeshi au viashiria. Urejeleaji katika Kiswahili unadhihirika kupitia kwa matumizi ya viwakilishi nafsi na vimilikishi, vivumishi vimilikishi, viashiria (vikitumika kama viwakilishi au vivumishi) na vielezi na vivumishi vya ulinganifu. Pia virejeshi ni vitambulishi vya urejeleaji katika matini. Hivyo kwa kuongozwa na nadharia ya Ushikamani inayosema Ishara na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wa maana na kila mmoja ndani ya muktadha wa lugha, Huu ni muhimili wake. Kwa mfano, sentensi nzima inapaswa kuwa na uhusiano wenye maana na maneno yake yote, na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wenye maana na vitu vinavyowakilishwa.

#### 3.2.2 Kuleta Muungano

Data zilionyesha dhima hii imeweza kuibuliwa kutokana na ushikamani wa kisarufi ambao ni ushikamani wa kisarufi ni ubadala. Aidha kibadala hicho huwa cha elementi nyingine ambapo hujitokeza badala ya kuirudia elementi iliyotangulia. Hivyo katika ubadilishaji huwa kuna uhusiano wa elementi za kisimu kama vile maneno na virai katika sentensi au matini.

Matokeo yalionyesha uunganishaji huu unahusu matumizi ya viunganishi kama vile "*na*," "*lakini*," "*kwa sababu*," na "*hata hivyo*". Ili kuunganisha sentensi na aya, na kuonyesha uhusiano kati ya mawazo tofauti. Viunganishi husaidia kuonesha iwapo mawazo yanakubaliana, yanapingana, au ni sababu ya mengine. Hivyo matokeo yaliendelea kuonyesha Viunganishi hutumika kuunganisha uhusiano wa kisemantiki kati ya sentensi iliyotangulia na ile inayofuta katika matini. Uunganishaji pia hutokea katika sentensi moja ikiwa kiunganishi kinaunganisha dhana inayotokea katika kishazi tangulizi na kile kinachofuata katika sentensi hiyo moja. Mfuatilizo wa wakati katika sentensi moja au mbili huwa kipengele cha mshikamano kwa sababu ya uhusiano wa kisementiki unaounganisha dhana mbili. Mfuatilizo huu huweza kuonyeshwa na kielezi. Kwa kuongozwa na nadharia ya ushikamani tunaweza kuona kuwa katika uunganishaji huu hali ya vipashio fulani (katika sentensi au matini) kukaa pamoja kwa uimara kama ilivyoweza kushadadiwa na Finch, (2000). Anasema kuwa ili matini, yoyote iweze kuwa na maana na kueleweka na wasomaji, lazima iwe na ushikamani. Tuliweza kuupata katika kijenzi hiki cha uunganishaji.

#### 3.2.3 Husaidia Kuleta Uwekevu Katika Matini

Data zilionyesha dhima iliyotokana na kijenzi cha udondoshaji ambapo hutoa baadhi ya maneno na kuacha mengine bila kuathiri maana katika matini mbalimbali, ili uweze kusaidia katika kuleta hali ya uwekevu katika matini.

Matokeo yalionyesha udondoshaji huu unahusu kuacha sehemu fulani za sentensi ambazo zinaweza kueleweka bila kuzitaja moja kwa moja kwa sababu zinajulikana kutoka muktadha. Udondoshaji husaidia kuepuka urudiaji na kufanya maandishi kuwa mafupi na

wazi. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kuwa udondoshaji ni hali itokeayo katika usemaji ambapo baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kisarufi huachwa bila ya kuathiri maana. Maneno haya hudondoshwa kwenye muundo wa sentensi na kuacha mapengo ya kimuundo. Wakati wa kufasiri maana, msomaji hurudia maneno haya kutoka sentensi zilizotangulia na kupata maana kamili. Hivyo kwa kuongozwa na nadharia ya ushikamani tumeweza kuona kuwa udondoshaji ishara na maneno yanapaswa kuwa na uhusiano wa maana na kila mmoja ndani ya muktadha wa lugha.

### 3.2.4 Kuleta Mpangilio Mzuri wa Mawazo

Data zilionyesha dhima inayojitokeza kutokana na kijenzi cha uunganishaji ni kusaidia kazi mbalimbali za kifasihi kuungana na kuleta mtiririko wenye kueleweka kwa wasomaji. Ushikamani wa kisarufi husaidia kuunganisha sentensi moja na nyingine kwa njia inayofanya maandishi kuwa na mtiririko mzuri na wa kueleweka. Hivyo dhima hii katika kijenzi hiki imeweza kusaidia katika kuunganisha neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi na mwisho sentensi na sentensi ili kupata mantiki kamili katika sentensi na matini kwa ujumla. Kwa ujumla Uunganishaji husaidia wasomaji kufasili uhusiano kati ya vishazi.

## 4.0 HITIMISHO

Katika sehemu hii ya hitimisho matokeo ya msingi makala haya yalijadiliwa. Mjadala huu ulilenga kudhibiti lengo mahususi la utafiti huu. Hivyo mjadala huu ulijadili matokeo yaliyopatikana kwa kuzingatia malengo mahususi, kulingana na data zilizopatikana katika sura ya nne. Katika kujadili matokeo yaliyopatikana mtafiti aliongozwa na nadharia ya Ushikamani ambapo tafiti tangulizi na kushadadia hoja kupitia wataalamu mbalimbali wa fasihi. Hivyo mjadala huu uliishia kwa kuona kuwa matini na kazi hizi za kifasihi huweza kuwa na ushikamani wa mawazo endapo vipengele vya darajia ya ushikamani wa kisarufi vitazingatiwa na kufuatwa, ili ziweze kuwa na ushikamani wenye kuleta mtiririko mzuri wa mawazo kwa kuwa kazi nyingi zikikosa ushikamani zinakosa maana iliyokusudiwa.

Makala hii inapendekeza kuwa watafiti na wataalamu wa fasihi wanapaswa kufanya tafiti nyingine kuhusu ushikamani na zifanywe kwa kutumia riwaya nyingine au kazi nyingine za waandishi hawa, ili kuangalia kama matokeo yake yatakuwa sawa na matokeo ya utafiti huu au yatatofautiana.

## MAREJELEO


- Barongo, S. O. (1996). *"Dhima ya Ushikamano Katika Utendaji Kwenye Insha za Kiswahili za Wanafunzi wa Kidato cha Nne, Wilayani Kisii, Kenya".* Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. Tasnifu ya M. Phil (Haijachapishwa).
- Chang, Y. (2012). A Tentative Analysis of English Film Translation Characteristics and Principles. *Theory and Practice in Langugae Studies ktk Academic Publisher Manufactured. Finland, 2*(1), 71-76.
- Ching-Ting, L. (2010). *"Analysis of English Subtitles Produced for the Taiwanese Movie Cape No. 7".* Auckland University of Technology (Tasnifu ya Uzamili - Haijachapishwa).
- Cronin, M. (2009). *Translation Goes to the Movies.* New York: Routledge.
- Finch, G. (2000). *Linquistic Terms and Concepts, London*: Macmillan.
- Halliday, M. A. K, Hassan R. (1976). *Cohesion in English*, Longman. London.
- Halliday, M. A. K. na Hassan, R. (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London.
- Halliday, M. A. K. (1985). *An Introduction to Functional Grammar, London*: Edward Arnold. Kenya.
- Koolstra, C. M., Peeters, A. L., & Spinhof, H. (2002). *The Pros and Cons of Dubbing and Subtitling ktk European Journal of Communication, 17*(3), 325-354.
- Makoti, V. S. (2013). *Mshikamano wa Kisarufi katika Kiswahili.* Nairobi: Chuo kikuu cha Moi.
- Mbatiah, M; (2001*): Kamusi ya Fasihi. Nairobi*: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mogadam, L., & Shabanipoor, M. (2013). Application of Ellipsis and Lexical Cohesion in Subtitling and Dubbing: The Case of Prison Break TV Series. *Journal of Foreign Language Teaching and Translations Studies*, 2(2), 70-90.
- Mkude, D. J. (2005). *The Passive Constructions in Swahili.* Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).
- Msokile, M. (1993). *Uchambuzi na Uhakiki: Karibu Ndani*. Dar es Salaam: DUP.
- Munyua, J. G. (1992). *"Uwakilishaji wa Nomino Katika Kiswahili*" Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Tasnifu ya M.Phil (Haijachapishwa)
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi ya Fasihi* ( Toleo la kwanza ). Rock Island IL: Augustina.
- O'Grady, W. na wenzake (1996) *Contemporary Linguistics: An Introduction, Harlow Essex*: Longman.
- Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi:* Dar es salaam. Karjaner Print Techinology.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Salkie, R. (1995). *Text and Discourse Analysis. London*: Routledge.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Thompson, E. (2004). *Manipulation of Verbal Inflection in English and Spanish Spontaneous Speech Error*. Ms. Florida International University.
- Toolan, M. (1998). *Language in Literature. London*. Cambridge Unversity Press

- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers. 248.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd. Nairobi Kenya.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher.
- Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd
- Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Vide _muwa, Nairobi.


**Cite This Article:** Allen Estomih Makyara & Neema George Mturo (2024). Ubainishaji wa Dhima Zilivyojitokeza Kupitia Vipengele vya Ushikamani wa Darajia ya Kisarufi Kupitia Tamthiliya ya *Natala* na *Morani*. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, *7*(12), 436-443.